

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

Telegram “**AFYA**”, DODOMA
Namabari ya Simu: **+255 026 – 2323267**



Mji wa Serikali Mtumba
Barabara ya Afya
S.L.P. 743,
40478 DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

MWENENDO WA UGONJWA WA CORONA (COVID-19) NCHINI

Dar es Salaam, Jumatatu Aprili 13, 2020

Wizara inatoa taarifa ya ongezeko la wagonjwa **kumi na nne (14)** wa Corona (COVID-19) nchini hadi kufikia **46 kutoka 32** tuliowatolewa taarifa ya awali tarehe 10 Aprili, 2020.

Wagonjwa wapya 14 wote ni Watanzania. Kati ya hawa wagonjwa walioko **Dar es Salaam ni 13** na **mmoja (1) yuko Arusha**. Wagonjwa wote wanaendelea na matibabu chini ya uangalizi wa wataalam wa afya. Ufuatiliaji wa watu waliokuwa karibu na wagonjwa unaendelea.

Kwa mara nyingine Serikali inarudia tena kuwasisitiza wananchi kuchukua tahadhari ya kujikinga na ugonjwa huu kama tunavyowapatia taarifa na elimu mara kwa mara kupitia njia mbali mbali na hususan kuepuka misongamano na mikusanyiko isiyokuwa ya lazima.

A handwritten signature in green ink, appearing to read 'Ummu Mwalimu'.

Ummu Mwalimu (Mb)

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,
JINSIA, WAZEE NA WATOTO**